**Jina: ..…………………………………………………………… Nambari.:……………………...............**

**Shule.: ………………………………………………………. Sahihi:……………………......................**

**Tarehe:…..……………..…………………………….....................**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**JULAI/AGOSTI - 2015**
**MUDA: SAA 2 ½**

# MTIHANI WA TATHMINI YA ENEO LA GATUZI LA TRANS-NZOIA

***Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**SAA 2 ½**

**MAAGIZO**

- Andika **Jina lako** na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia **sahihi yako** kisha uandike **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali **yote** katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha majibu.
- Hakikisha kwamba kurasa zote zimepigwa chapa.
- Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.**

**Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee**

| SWALI/SEHEMU | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |

*Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa.*
*Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa*
*na kuwa maswali yote yamo.*

**1. UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali :-***

Ingawa wenye hekima walisema kuwa macho hayana pazia, ni muhimu kuyatumia macho ulivyojaaliwa na muumba wako. Ndio maana ninaamini pia kuwa macho hayafilisi duka ! Mimi hupenda kuyafumbua macho pima kila nitembeapo barabarani au hata ninapokaa nyumbani kusakura yaliyo karibu nami. Lakini kuna matukio ambayo hunisumbua na kunisikitisha. Hunisumbua kwa sababu sipati majibu kwayo ; hunisikitisha kwa sababu ya athari zake na mihemko yanayoleta katika hisia zangu za ndani. Kila mara hujiuliza : "Kwa nini watu wengi huteseka namna hii duniani ? Kwa nini mtu adamke mafungulia ng'ombe akielekea kibaruani kila siku bila kusita huku wachache wakistarehe ? Kwa nini ugonjwa unaweza kumvamia mtu ghafla bin vuu na kumlemaza ama kumtaabisha kwa muda mrefu kabla ya kumuua ? Kwa nini ? Mbona kila mara mtu anapokuwa akisikitika, kuna mwenzake huwa anacheka ? Ama maisha ni kitendawili tu ?

Hata hivyo, linalonishangaza sana wakati mwingine ni jinsi wale ninaowafikiria kuwa wanataabika wanavyochukulia hali zao. Utawaona akina yakhe wakitabasamu kila mara na kucheka hata matumbo yakiwaguruma. Utawasikia wakiulizana : "Umeshindaje ?" Kana kwamba wamejishindia chochote kwani unapoangalia vizuri unakuta kwamba wameshindwa karibu kwa kila hali. Mbona wasiulizane : Umeshindwaje?

Hii ndio sababu wakati mwingi moyo wangu huanza kuhisi kuwa labda siku ya kiyama inakaribia zaidi. Wewe hebu fikiria, wanasayansi wanapotuambia kila mara kuwa wamevumbua hiki ama kile ambacho kitafanya maisha ya wanadamu kuwa rahisi zaidi, ndivyo tunavyojitumbukiza katika majanga na matatizo zaidi maishani. Hii ndio sababu hata ile dhana iliyokuwepo miaka ya nyuma kuwa maradhi ya Ukimwi ambayo yamekosa tiba hadi sasa kando na kuwaua mamilioni ya watu yalitokana na ajali ya kisayansi huko Marekani inaweza kupata mashiko.

Swali la kujiuliza ni : "Ni kwa nini maisha yanaposemekana kuwa yamebadilika na kuwa mazuri Siku hizi ikilinganishwa na zamani mimi naona kinyume ? Au wewe waonaje ? Mbona zamani kabla ya majilio ya kile siku hizi kinaitwa'maendeleo ' watu walikuwa wakitembea tu na kula matunda namimea, watoto wakicheza na kucheka kwa furaha bila bughudha yoyote ? Au hata mbona watu hawakuwa na ubinafsi niuonao siku hizi?"

Maendeleo hayo tunayotaja kila siku nayaona kama ongezeko la chuki, magonjwa, ubinafsi, vita, ufisadi na hujuma dhidi ya mazingira ambamo mwanadamu anafaa kufurahia maisha. Ukweli ni kwamba maendeleo hayo yamepelekea watu wengi zaidi ulimwenguni kuishi katika mitaa ya mabanda, kuwa na nyuso za "Sitaki mchezo" na "karibu lakini usidowee". Ninapozama zaidi katika bahari ya luja kuhusu hali hii ya duniani ndivyo ninavyochanganyikiwa zaidi kuhusu ukweli halisi. Maajuzi nimeishitakia hali hii kwa Mola ingawa sijajaaliwa jibu. Hata hivyo, ninavyoendelea

kulingoja jibu ndivyo ninavyoendelea kuelewa ile dhana kuwa ulimwengu ni kokwa ya fuu huishi utamu, anayekwisha ni binandamu.

***Maswali***

(a) Tolea makala haya kichwa mwafaka. (alama.1)

……………………………………………………………………………………………………

(b) Kwa nini mwandishi anadai kuwa labda siku ya kiyama imefika ? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(c) Unafikiri ni kwa nini mwandishi anayaona madai kuhusu maendeleo duniani kuwa nikinaya? (alama 3)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(d) Mwandishi wa taarifa anamaanisha nini kwa kusema :

(i) Sitaki mchezo

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(ii) Karibu lakini usidowee. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(e) Yalinganishe maisha ya kabla ya maendeleo na ya sasa ambayo mwandishi anadai ni duni kuliko ya zamani (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(f) Je, unakubaliana na msimamo wa mwandishi kuwa madai kuhusu maendeleo ni kinaya? (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

(g) Eleza maana ya vifungu vya maneno kama vilivyotumika katika taarifa. (alama 3)

(i) Kusakura ……………………………………………………………………………………

(ii) Bahari ya luja………………………………………………………………………………..

(iii) Ulimwengu ni kokwa ya fuu huishi utamu, anayekwisha ni binadamu.

……………………………………………………………………………………………………

**2. MUHTASARI**

***Soma taarafa ifuatayo kisha ujibu maswali***

Miongoni mwa starehe ambazo Waswahili wamezihifadhi mpaka leo ni kutoleana hadithi na kutegeana vitendawili. Starehe hizo ambazo kwa kawaida hufanywa nje huwa njiani au uani, ama ndani chumbani au ukumbini, aghalabu hufanywa wakati wa magharibi au usiku baada ya kila mtu kumaliza kazi za nyumbani, dukani, shambani, ofisini na kadhalika. Mambo haya yakitazamwa sana itaonekana kuwa hayakufanywa vivi hivi.

Tangu zamani wazee wa Kiswahili waliwakataza wana wao kucheza mchana. Hawakupenda vijana wajizoeshe uvivu kwa kupiga malapa. Walisadiki kuwa mwana ambaye hakukanywa dhidi ya utiriri huu hangeweza kujifaa yeye mwenyewe na wala hata watu wengine. Isitoshe nani asiyejua kuwa ajizi ni nyumba ya njaa? Vijana walihimizwa kusaidia katika makazi mbali mbali yanayofanywa majumbani, mashambani na mahali popote palipohisiwa kuwa mtu angalifanyiwa jambo la kumpa riziki. Ndiposa ungesikia wazee wakiwaambia watoto wao,'ukisimulia hadithi mchana utaota mkia'. Ingawa kwa watu wazima maneno haya yangekuwa masihara, kwa watoto yaliaminika sana kwa hivyo wazazi wakapata mradi wao. Hi ndiyo maana Waswahili wanasimuliana hadithi na kutegeana vitendawili jioni au usiku.

Wazazi ambao hawataki watoto wao watembeetembee au wacheze michezo ambayo itawafanya wakimbiekimbie na kujihasiri huwatia ndani ili wawe nao kuanzia magharibi. Waswahili wana itikadi nyingi zinazohusiana wakati wa magharibi. Ni ajabu kuwasikia wakisema kuwa magharibi huwaleta pamoja na kutoleana hadithi. Na hata kama si hivyo hii ni fursa nzuri kwa wazazi kuzungumza na watoto wao ambao kutwa nzima huwa hawakupata nafasi kuwa nao.

Starehe hizi pia huongeza elimu, na kama wahenga wasemavyo, elimu ni mwanga uangazao.. Kwa mfano watoto watategewa vitendawili, jambo hili litawafanya wafikiri. Na kufikiri huku kutawafanya wavumbue mambo mengi ambayo mengine hapo awali hawakuyajua na kuyathamini. Vile vile huwafunza werevu wa kufumba na kufumbua mafumbo ambayo ni elimu inayohitaji kiwango kikubwa cha busara.

Kutoleana hadithi ni miongoni mwa starehe ambazo kwazo hujifunza mambo mengi sana. Katika hadithi watoto wanaweza kujifunza mambo yanayohusu mila na desturi, katika mambo haya watu hujifunza tabia nzuri, heshima, uvumilivu. Pia katika hadithi mtu anaweza kujifunza mambo ya historia na pia ya mazingira aliyoyazoea na hata mambo ambayo hayajui.

Aidha hadithi ni chombo ambacho wazee hukitumia kuwafundisha watoto mbinu za kuzungumzia. Wazee wenye busara aghalabu huwapa nafasi watoto wao wabuni na wasimulie hadithi zao. Wakati mwingine jamaa mbili jirani huweza kukutana kufanya mashindano ya kutambiana hadithi. Mazoezi kama haya huwawezesha vijana kufikia viwango vya juu vya ufasaha na matumizi ya lugha na ujasiri na ukakamavu wa kuweza kusema mbele za hadhira kubwa katika maisha yao. Baadhi ya watambaji wakubwa waliopata kusifiwa haikosi mwanzo wao ulikuwa wa namna hii. Hadithi pia

huwafundisha watu kuhusu maisha duniani. Zinaweza kuwafunza jinsi ya kuishi na ndugu, majirani, marafiki, wake au waume. Ulimwenguni humu tunamoishi mna mambo mengi yanoyomtatiza binadamu kwa namna mbalimbali. Hadithi zinaweza kupendekeza mambo ya kufanya na kuonyesha njia zenye mapato mema tunapofikiwa na adhawa kadha. Zinaweza pia kukanya kiburi na kuonyesha faida ya kutosema uwongo ama kuishi katika maisha yasiyo muruwa, yaliyojaa kiburi na majivuno. Hapana shaka hadithi zinaweza kuongoza na kuwafanya wawe watiifu na raia wema katika nchi zao.

***Maswali***

a) Kwa nini mwandishi akaoanisha utambaji wa hadithi na wakati wa jioni? (Maneno 40) (al. 5)

**Nakala chafu**

……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..

**Nakala safi**

……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..

b) Kwa maneno kati ya **70 na 90** eleza umuhimu wa kutambiana hadithi na kutegeana vitendawili, kulingana na mwandishi. (al. 17)

**Nakala chafu**

……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………..

**Nakala safi**

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

**3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**

(a) Eleza sifa **mbili mbili** za sauti zifuatazo**.** (al. 2)

(i) /i/………………………………………………………………………………………...

…………………………………………………………………………………………….

(ii) /o/ ……………………………………………………………………………...….

…………………………………………………………………………………………….

(b) Onyesha mahali mkazo unapowekwa kwenye neno ‘Tenganisha’. (al. 1)

……………………………………………………………………………………………..

(c) Eleza matumizi **manne** ya kiimbo. (al.2)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(d) (i) Eleza dhana ya mofimu. (al. 1)

……………………………………………………………………………………………..

(ii) Huku ukitolea mfano, taja aina **mbili** za mofimu. (al. 2)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(e) Ainisha vipengele vya kisarufi katika sentensi hii.

Aliyekusamehea ........................................................... (al.3)

……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………..

(f) Ainisha nomino katika sentensi hii.

‘Juma, na jeshi lote walikula chakula cha raha’ (al.2

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(g) Andika kwa udogo wingi. (al.3)

'Njia hii yetu inapitiwa na mtu mnene.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………..

(h) Bainisha aina za vishazi katika sentensi hii. (al.2)

'Katiba ambayo inapingwa na wengi haitetei maslahi ya walio wachache'

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

(i) Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo. (al. 1)

'Alipiga mpira teke ukaruka juu juu zaidi.'

…………………………………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………………………………...

(j) Changanua sentensi hii kwa kutumia kielelezo cha matawi. (al.4)

"Tulimtembelea mgojwa jana hospitalini"

(k) Tumia kireshi 'O' tamati katika sentensi ifuatayo. (al.2)

'Kalamu ambayo alinunua ni ile ambayo anaipenda.'

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(l) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.

"Msiposoma kwa bidii wakati huu, mtaanguka mtihani mwaka ujao."Mwalimu akawaambia wanafunzi wake. (al.3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(m) Tunga sentensi ukitumia kitenzi kifuatacho kauli ya kutendeka. (al.2)

'nywa.'

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(n) Eleza matumizi mbalimbali ya "ni" katika sentensi ifuatayo. (al. 4)

'Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani.'

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(o) Tunga sentensi **moja** kuonyesha tofauti ya kimaana kati ya 'Husuni' na 'Huzuni.' (al.2)

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(p) Tunga sentensi kwa kutumia vihisishi vifuatavyo. (al. 2)

(i) Alhamdulilahi

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(ii) Laiti

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(q) Eleza maana **mbili** za sentensi hii. (al. 2)

Alinichezea na Baniani

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

## 4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

**Karua**: Mheshimiwa Spika, naomba nipewe fursa kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa Bungeni na mbunge wa Cherengany mheshimiwa Isaac Salat ……………………....

(a) Yaweke makala haya katika muktadha wake. (al.1)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(b) Eleza sifa za mazungumzo yanoyofanywa katika muktadha huo uliotaja. (al. 4)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

(c) Eleza sababu **tano** zinazowafanya watu kubadili msimbo. (al. 5)

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................

.......................................................................................................................................